



REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI
THIRD ASSEMBLY-THIRD SESSION

THE HANSARD

Monday, 10th June 2024

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2:30 p.m.*

[The Deputy Speaker (Hon. Kombo) in the Chair]

PRAYER

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

WELCOMING MEMBERS FROM THE LONG RECESS

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Maybe on Communication, just to welcome all the Members back to business in this honourable House. I believe we had an awesome recess, so *karibuni sana*. Next Order!

PAPER LAID

SECOND QUARTER REPORT FOR THE DEPARTMENT OF PUBLIC WORKS, ROADS AND TRANSPORT

Hon. (Ms.) Koki: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to lay the following Paper on the Table: -

The Second Quarter Report for the Department of Public Works, Roads and Transport.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Hon. (Ms.) Koki laid the document on the Table)

STATEMENT

BUSINESS FOR THE WEEK COMMENCING MONDAY, 10TH JUNE 2024

Hon. Ngirani: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I hereby stand to go through the Order of business for the week. That is on Monday, June 10th, 2024, at 2:30 p.m. We have: -

- A. Papers; the Second Quarter Report for the Department of Public Works, Roads and Transport. That has already been done by our Deputy Leader of Majority.
- B. We have Statements: Response to a Statement sought by hon. Naftali Nyae Kombo regarding Kwa Kijala and Kawala boreholes. Response to a Statement sought by Hon. Mohammed Mwambire regarding Governor's Cup prizes from the Department of Gender, Culture, Social Services, Sports and Disaster Management.

On Tuesday, June 11, 2024, at 9:30 a.m. we have: -

- A. Papers; Report on the implementation status of an Assembly Resolution Regarding Youth Economic Empowerment (*Kazi Kwa Vijana* Programme) from the Department of Gender, Culture, Social Services, Sports and Disaster Management.
- B. We have Statements: Response to a Statement sought by Hon. Naphtali Nyae Kombo regarding Chadi-Mikomani-Dzanikeneni Road.

On Tuesday, June 11, 2024, at 2:30 p.m. we have: -

- A. Papers: Report on the implementation status of an Assembly Resolution on the Report of the Sectoral Committee on Roads, Transport and Public Works on the status of Roads for FY 2021/2022 presented by the Leader of Majority. Two, we have the Kilifi County Youth Development Policy 2022-2026 from the Department of Gender, Culture, Social Services, Sports and Disaster Management.
- B. We have Statement: Response to a Statement sought by Hon. Samson Zia Kahindi regarding Budget absorption for the FY 2023/2024 from the Department of Finance and Economic Planning.

On Wednesday, May 12th, 2024, at 2:30 p.m. we have: -

- A. Papers: Physical and Land Use Plan for Vuma Trading Center PDP No.883.KLF.1.2019 by the Leader of Majority.
- B. We have a Response to a Statement sought by Hon. Mohamed Mwambire regarding Road Maintenance Kitty from the Department of Transport and Public Works.

Thank you, Mr. Speaker, Sir.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Thank you. So, we have an intervention from hon. Benson Karisa Ngirani.

MOTION FOR ADJOURNMENT

INDEFINITE ADJOURNMENT OF PLENARY SITTINGS IN SOLIDARITY WITH HON. TETE WHO IS CURRENTLY IN POLICE CUSTODY

Hon. Ngirani: Thank you, Mr. Speaker. Again, I rise Pursuant to the Provisions of Standing Order 28 read together with Standing Order 50 (b) to move: -

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

THAT, this County Assembly do now adjourn its Plenary Sittings indefinitely.

Mr. Speaker, before I call upon the seconder of this Motion, this Motion is regarding our colleague who is the representative of Shimo la Tewa Ward hon. Haron Tete, who happens to be our Majority Whip.

Mr. Speaker, this House and all Members are aware that hon. Tete at the moment is in police custody and with that solidarity, we the Members of this County Assembly feel that as we are here, we are representing different wards but we feel that Shimo la Tewa is not represented in this House. To be fair, the people of Shimo la Tewa are supposed to be represented as we resume the sittings of this House. Therefore, we feel that we adjourn this House indefinitely until that time when the leadership of this House, the leadership of this County Assembly and the leadership of the County Government of Kilifi together make efforts for the release of hon. Tete. With those few remarks, I am calling upon hon. Betty Kache to second this Motion. Thank you.

Hon. (Ms.) Betty: I second.

(Question proposed)

Hon. (Ms.) Koki: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me this opportunity to support the Motion on the Floor that we adjourn this House so that we can be able to stand together with our Majority Whip. I stand to support this Motion so that we can get to the details or understand what is happening because the people of Shimo la Tewa are not represented in this House and we want to know the safety of our colleague who is an hon. Member and the Majority Whip of this House. So, I support it.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Hon. (Ms.) Meso.

Hon. (Ms.) Meso: Thank you, Mr. Speaker, Sir. First, I thank the Almighty God for guiding us after the long recess. It is quite unfortunate it ended in a very bad, awkward way without our Chief Whip who has been arrested. I support this Motion, but I am wondering what is really happening in Kenya because hon. Tete is still innocent, he is not guilty but why is it that they do not want him to take bail so that he can be out and go to court? Is there anything hidden? We would really like to know, and I beg this House if it is going to continue this way, I think we should have a very big demonstration from Kilifi County Assembly to Shimo la Tewa Prison.

It is awkward and they have to explain to us what is really happening because right now we do not know if it is true that he did it. We do not know; it is just hearsay. Some people say there are no eyewitnesses. What is happening? Shimo la Tewa now does not have any representative. We are now having 34 wards. I really support this Motion, and we have to organize a demonstration. Thank you.

Hon. (Ms.) Betty: Asante sana, mheshimiwa Spika. Nami niungane na waheshimiwa wenzangu kwa Hoja ambayo mheshimiwa Ngirani ameuleta.

Mheshimiwa Spika, sisi ambao tuko hapa ni wajumbe waliochaguliwa na wananchi na sisi pia tuliteuliwa na vyama tuko hapa ili kuwakilisha watu wetu. Wakati wowote mtu akitaka kupigania haki kwa watu ambao wako na umaarufu ama mabwenyenye anaonekana ni muongo. Hatutaishi kwa vitisho vya mabwenyenye katika Kilifi yetu kwa sababu tuna haki ya kutetea wananchi wetu.

Tungelitaka kuliweka hili wazi, yale aliyoongea mheshimiwa Meso ndio ambavyo itakuwa maanake subra yetu saa hii imeisha. Leo kama sio siku ya nne ni siku ya tano Shimo la Tewa haina Mwakilishi. Mwakilishi wao ako kizimbani sababu ambayo inamfanya yuko

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kizimbani ni kwa ajili ya kusimama na wananchi wake. Swali ni; sisi tuliletwa hapa Bunge kuwakilisha wananchi wetu ama tuliletwa Bunge kwa mikono ya mabwenyenye? Kwa sababu sisi kama Wawakilishi katika Bunge hili tukitaka kuwakilisha watu wetu tumeekelewa maneno ambayo hayakufanyika. Ninaongea hivi nikiwa na uchungu kwa sababu pia mimi niko na hofu. Leo ni mheshimiwa Tete kesho ni mimi. Hatuko tayari kunyanyasika kwa sababu tunajua haki na ni kitu gani tunakifanya.

Mheshimiwa Spika, sio kwamba ni vitisho tunatoa lakini kama hatutapata haki kwa Mheshimiwa Tete hii Kaunti ya Kilifi itasimama. Hakuna kitu ambacho kitaendelea, hakuna mtu ataingia Kaunti hii na hakuna mtu atatoka Kaunti hii.

Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, sisi tunapotoka hapa na kufunga hili Bunge, tunataka haki itendeke kwa wenzetu. Tunataka haki, tunaitisha haki kwa sababu ana haki kama binadamu yoyote.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa mwingi wa maneno kwa sababu nasikia vibaya mtu anajaribu kutetea haki anaonekana ni muongo. Mheshimiwa Spika, hawa wajumbe ambao wako hapa mimi nawaomba kwa sababu kuna macho mabaya huko nje. Kuna watu wenye nia mbaya na uongozi wetu. Hivyo basi, tusali sana na tuamini kuwa kila kitu kinawezekana mbali na kuwa tunatetea haki zetu, pia tumueke mikononi mwa Mwenyezi Mungu wenzetu ambaye yuko pale kizimbani. Asante sana, mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante sana, mheshimiwa Betty Kache. Twende kwa mheshimiwa Twaher.

Hon. Twaher: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa fursa hii. Kwanza, ni jambo la kusikitisha sana kwamba mheshimiwa alipelekwa mahakamani. Upande wa washtaki waliomba mahakama waendeleo kumzuia kwa ajili ya uchunguzi. Hii ni mbinu ambayo inatumika kutishia ama kuhujumu harakati za watetezi wa haki za wanyonge. Vitisho, mheshimiwa Spika, nataka vikae wazi na wakaazi wa Kilifi na Taifa kwa ujumla wafahamu kwamba hatutarudi nyuma kutetea watu wetu katika haki za mashamba na ardhi ambazo zinanyakuliwa.

Mheshimiwa Spika, mambo ya ardhi ni mambo ambayo yamekithiri katika Kaunti yetu ya Kilifi. Unyakuzi umekuwa wa hali ya juu. Mheshimiwa Tete tunakaa naye pamoja katika Kamati ya Ardhi. Alikuwa ametembelea eneo ambalo liko kwake kujua matatizo yalio pale ili awasilishe katika Kamati ya Ardhi ili tuweze kufwatilia. Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya hakuna ushahidi wowote wa kuwa mheshimiwa Tete alihusika katika mauaji wa mtu mmoja ambaye alifariki siku hiyo.

Mheshimiwa Tete amezuiliwa gerezani, amenyimwa bondi ili aendeleo kukaa ndani ya korokoroni ili watu wengine ambao wanahusika katika kutetea ardhi hiyo wote waingie hofu. Ikiwa mheshimiwa atazuiliwa ndani, je mwananchi wa kawaida itakuwa namna gani? Sisi tunasimama kidete na hili tatizo haliko katika Wadi ya Shimo la Tewa, nina imani wadi karibu zote kwa Kaunti yetu ya Kilifi kuna matatizo ya ardhi na hatutatishwa na polisi wala DCI (*Directorate of Criminal Investigation*) wala kitengo chochote cha Serikali ambacho kinatumika ili kuzuia haki isifanyike.

Ningependa kuwaomba Wajumbe wenzangu siku ya korti sisi sote kwa umoja wetu tufike pale kortini na ikiwa siku yake ya kufikishwa mahakamani *application* ifanywe mheshimiwa Tete aweze kuachiliwa kwa dhamana yenye kuonekana. Wasiweke dhamana kubwa ambayo ina muumiza kwa sababu yeye ni kiongozi ambaye amechaguliwa na watu. Mheshimiwa Tete hangekimbia mahali popote lakini mahakama imetumia sheria mbaya ya kumzuilia korokoroni ili kuweka vitisho. Mimi nasema tuweke bayana kwamba vitengo vya serikali

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

visitumike vibaya kuumiza wanaharakati wa kutetea haki za mashamba za watu wetu. Naunga mkono kuhairishe vikao mpaka haki ya mwenzetu ipatikane. Asante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante, mheshimiwa Twaher, kwa changizo zako. Twende kwa Mheshimiwa Thaura.

Hon. Thaura: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi hii pia nichangie katika Hoja ambayo ipo kwenye Sakafu.

Mheshimiwa Spika, naungana na waheshimiwa wenzangu wanaounga mkono Hoja hii kwamba tusitishie vikao hadi pale mwenzetu wa Shimo la Tewa atakuwa huru. Swala la ardhi Kilifi Kaunti ni nyeti sana na kama ndugu zangu waliotangulia kuongea ni kwamba kwa kumzuilia Tete ni njia ya kunyamazisha wana Kilifi katika harakati zao za kupambana na mabwenyenye ambao wamekuja kunyakua ardhi. Inatumika kama njia ya kutia hofu ili kiongozi yoyote ama mwananchi mwenye nia safi awe ataogopa kuingia katika mchakato huu. Ni vizuri ieleweke Kenya nzima kwamba leo tumeamua kwa sauti moja kama viongozi wa Kilifi tunasimama na ndugu yetu sio tu kwa sababu ni mmoja wetu hapa Bunge mbali yeye ni kiongozi na ni mwana Kilifi na hatutakubali hujuma ambayo inafanyika kuhujumu watu wanaotetea haki za wana Kilifi.

Serikali itakuwa inazembea sana kwamba maswala ya ardhi Kilifi bado hayajachukuliwa na uzito. Mutaniruhusu kusema yale yanayoendelea kisiasa. Hata baadhi ya wale viongozi ambao wako katika serikali ya Kenya Kwanza bado wanalalamikia kukosa kuwajibika kwa serikali wanayoifanyia kazi. Kuna mtu amelala katika kazi yake, hii ni “*wake up call*” kwamba sisi wana Kilifi na kama viongozi tutasimama ili kuhakikisha kwamba haki inapatikana na sio tu kwa ndugu yetu mheshimiwa Tete, kuanzia sasa sisi wana Kilifi tutakuwa tunasimama kutafuta haki. Tuko sahihi kusitisha vikao kwa niaba ya mmoja wetu na bado ni mwana Kilifi.

Hon. Kea: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I stand in solidarity with hon. Tete, who is currently in custody in Shimo la Tewa Maximum Prison.

Mr. Speaker, Sir, this is a deliberate attempt to frustrate the efforts of Kilifi leaders to fight for their people and we cannot allow it. Hon. Tete is the Chief Whip of this House, whose main duty is to make sure that this Assembly works properly by attending sessions, so if he is absent, whom do they think is going to represent him in the House?

Hon. Tete is a representative of Shimo la Tewa, it takes somebody whose mind has gone bizarre to go and kill his electorates. I do not know which law they used to deny him bail because he is still innocent until proven guilty. We read something sinister when we went to the Shanzu Law Court. His case did not appear on the case list of that day. Members of the Assembly were frustrated because we did not know the time the case was coming to the court. I want to send a wake-up call, we are not going to be intimidated or frustrated, we are going to work around the clock to make sure hon. Tete is out.

If peace will have to prevail in Kilifi, Hon. Tete must be out. I concur with the Motion which has been brought by hon. Ngirani with immediate effect, we suspend the sittings of this honourable House until we Hon. Tete is out. I support the Motion.

Hon. Munyoki: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa fursa hii. Nasimama kuungana na wenzangu kumtetea ndugu yetu hon. Tete.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka tulishinda na wewe siku ya Alhamisi kuanzia saa mbili na nusu hadi saa saba bado tukitafuta mashtaka ya mheshimiwa Tete. Ni kama walikuwa wanapanga asijitokeze ili wamshike. Jambo la kushangaza ni kuwa baada ya kung’ang’ana kumtetea bado waliamua kumweka ndani. Sioni sababu ya kumzuia, walikataa kumpa fursa ya

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kuwa inje na kuendelea kusikiza vikao vya hayo mashtaka. Naunga mkono na nawaomba wenzangu wote tuisitie hapa, maana swala la ardi ni donda sugu Kilifi Kaunti nzima. Tuwe na mawazo ya kushughulikia swala hili la ardhi kando na Bungeni maana leo ni mheshimiwa Tete kesho ni mwingine, itaendelea kama hatutasitisha tabia hii. Naunga mkono kusitisha vikao hadi tujue mwelekeo wa kuhakikisha kuwa mheshimiwa Tete amewachiliwa.

Hon. Changawa: Asante, kwa nafasi hii. Nasimama kuunga mkono swala la kusitisha vikao hadi mheshimiwa atakapotolewa. Nataka kusema kwamba, tunaposoma katika Kitabu cha Warumi mlango wa kumi tano, mstari wa kumi na mbili unasema “furahikini na wale wanao furahi, lienii na wale wanao lia”.

Sisi kama Wabunge mmoja wetu anapopatawa na shida tunastahili kulia pamoja naye anapoingia katika furaha tunastahili kuwa katika furaha naye. Hata kwenye *Standing Orders*, sheria inasema tufwatilia wenzetu wanapokosa vikao. Hatutaki ihesabiwe kuwa mheshimiwa Tete anakosa vikao na yeye akiwa hayuko hapa. Nasema tufunge Bunge, tuende kusaidiana na mwenzetu mpaka maneno yatakapoisha. Maswala ya uuwaji katika maandamano hayaanzi kwa Mheshimiwa Tete, haya ni mambo ambayo yamekuwa yakifanyika. Ndani ya Kenya hii kuna watu wamekufa katika maandamano na hakuna kiongozi aliyefikishwa kortini kwa sababu kama hiyo na hata kunyimwa *bond*.

Sisi kama viongozi nataka kusema sio kwamba tunafunga tu pekee, bali tunahakikisha kwamba tuko pale usiku na mchana mpaka Tete atoke. Hatutasubiri siku saba, hizo ni zao sisi tunasema *it is now* ama sisi sote tuwe hapo ndani mpaka watakapoamua kumtoa.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Mheshimiwa Changawa pongezi, leo umetuvalia walahi na Kanzi ya bei ya juu lakini ukaingia kwenye Bibilia nafikiri tukikupa nafasi nyingine utarudi kwenye Quran. Asante na pongezi kwa hilo.

Hon. Rafiki: Asante sana, mheshimiwa Spika. Mimi nataka pia kuunga mkono mapendekezo ya mheshimiwa Ngirani. Kwa mtazamo wangu, mheshimiwa Tete hatendewi haki kwa sababu ni jukumu la mjumbe kutetea watu wake wakati watu wake wanapata matatizo. Sasa kama Kenya itafikia kiwango cha kwamba kiongozi akiwa anatetea watu wake ni ashitakiwe na hatia, sasa sijui twarelekea wapi. Imenishangaza kwa sababu mheshimiwa Tete ni mjumbe wa Wadi ya Shimo la Tewa. Ile wadi iko katika Kaunti ya Kilifi, kama ni makosa yalifanyika katika kaunti ya Kilifi, Kaunti ya Kilifi ina mahakama nyingi za kutosha, sielewi kulikua na mbinu gani mbali na uonevu uliosababisha mpaka mheshimiwa Tete asomewe mashtaka katika Kaunti ya Mombasa?

Lile shtaka lilifanyika katika Kaunti ya Kilifi, sio lazima kuwe kuna maonevu ya hali ya juu sana yale mheshimiwa anayofanyiwa. Iieleweke kwa kaunti kwamba hatuhairishi Bunge hili kwa sababu ya mheshimiwa Tete amezuiliwa, twayafanya haya kwa sababu watu wetu wa Kilifi wajue kwamba kama Wajumbe wa Kaunti hatuwezi kusokota mikono wakati watu wetu wanaendelea kuonewa na matatizo ya mashamba. Hivi vitisho vitafanyiwa Tete leo, kesho itakua mwingine; hatuwezi kuendelea namna hii. Namalizia nikisema kwamba, wacha tuahirishe Bunge hili mpaka haki za mheshimiwa Tete na watu wa Shimo la Tewa zipatikane. Asante sana, mheshimiwa Spika.

Hon. Juma: Asante, mheshimiwa Spika. Sisi kama wajumbe mbali na Wajumbe wa Kaunti, hata wale wa *National Government* tunaongozwa kisheria na tuko hapa kisheria. Kulingana na kipengele cha 27 cha Katiba yetu ya Kenya inazungumzia maswala haya ya kwamba hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kuvunja ukizingatia maswala ya katiba. Kila mmoja ana haki sawa, Mhindi, Mwafrika, Muingereza ana haki sawa na anastahili kuhudumiwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kisawa sawa. Katika vipengee kadha wa kadha katika sheria hiyo hiyo vinazungumzia mtu yeyote ambaye ataonekana akihujumu hiyo sheria basi mtu yeyote aweza kujitokeza na akaweza kutetea Katiba hii.

Ninachotaka kusema ni kwamba hakuna taarifa yeyote kwenye vyombo vya habari ambayo imeweza kuelezea mheshimiwa Tete amefanya utovu wa nidhamu katika sehemu tofauti tofauti. Tukiangalia Kenya na sehemu nyengine, kuna washukiwa wa maovu tofauti tofauti lakini wao pia huenda mahakamani kulingana na sheria na wakapewa *bond* na wakarudi nyumbani kisha uchunguzi utakua unaendelea hivyo hivyo.

Mheshimiwa Tete ni kiongozi ambaye tuna uhakika mkubwa sana japo ataondolewa arudishwe nyumbani na aendeleo na kazi yake hatoweza kuhujumu na kuenda mahali popote kulingana na kazi zake. Ninashangaa inasemekana mpaka muda fulani. Naomba wajaribu kupekua vipengee kadha wa kadha vya kisheria na waweze kumruhusu sasa hivi aweze kuendelea kisha wao nao waendeleo na shughuli zao za kufuatilio hilo.

Idara ambayo inaweza kusema huyu amefanya makosa ni jaji peke yake. Sawa sawa kulingana na Katiba yetu mheshimiwa Tete ni awachiliwe, uchunguzi ukiendelea na baadaye tutakubali uamuzi lakini kwa sasa hivi, mimi naunga mkono tusitishie hapa maanake si kwamba tunamtetea Tete peke yake lakini hata na Katiba. Asante.

Hon. Hinzano: Asante sana, mheshimiwa Spika. Tunasimama na mwenzetu kwa sababu hana hatia pale alipo mpaka mahakama itakapoamua baada ya uchunguzi. Ni huzuni kubwa sana kuona kwamba katika Jamuhuri yetu ya Kenya kuna baadhi ya sehemu ziko huru na nyengine bado hazijakua huru. Ni huzuni sana wananchi wa Jamuhuri ya Kenya tunaenda kwa siku kuu ya Jamuhuri na siku kuu ya Madaraka lakini hatujakua kwamba tuko katika jamuhuri ambayo iko huru na madaraka kamili ambayo tumekabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, itakuaje tulikua huru mwaka wa 1963 lakini baadhi ya sehemu katika Jamuhuri ya Kenya hazijakua huru kama hapa Pwani kwetu. Eti unaambiwa kuna mabwenyenye ambao wako mahali sijui *absentee landlords*; hawa *absentee landlords* wana urefu kiasi gani, wana ufupi kiasi gani, ni weupe kiasi gani, ni weusi kiasi gani, wanaishi bara lipi ambao hawatokei wakaonekana ili tukajua hizi ardhi zetu walizipata vipi katika Pwani hii yetu.

Ni huzuni kubwa sana na ni huzuni kwa sababu ukiifuatilia kwa makini utakuta huyu mumiliki wa hizi ardhi ana ekari zaidi ya 400 kuendelea. Walizipata vipi na sisi tumekua huru na hata kule sehemu za bara bara baada ya uhuru walikabidhiwa wale wenyeji wa kule. Itakuaje sisi tunaieleza kuhusu sijui kulikua na Mureno ama Mwarabu bado anamiliki ardhi hapa kwetu Pwani.

Ni huzuni kubwa sana na mimi naungana mkono na Raisi aliposema kwamba mahakama zetu zimejaa wakora. Maamuzi yaliyofanywa na huyu hakimu kumnyima dhamana mheshimiwa Tete, ni huyu hakimu ni mmoja katika wale wakora kwa sababu haiwezekani kumnyima dhamana mheshimiwa yuajua ana wakilisha wadi na hawezi kutoka kwa sababu ni mwakilishi wa wadi.

Mambo ya maandamano tumeyaona na kesi kama hizi zimekuwepo, mbona wengine wanapatiwa dhamana na wala sio mheshimiwa Tete? Hali hii ni lazima tuikomeshe na tutaikomesha kisheria lakini pia amani haiji ila kwa ncha ya upanga. Tumeona kwamba ni lazima jambo fulani lifanyike ndio watu wetu wawe huru. Hilo hatutasita, tatalitengeneza ili wananchi wa Pwani wawe huru. Pale kwangu Kakuyuni eti kuna bwenyenye sehemu ya Vihingoni na Malimo plot 446 na 447; mimi nataka niseme hivi, kama mambo haya ya mabwenyenye hayataisha mtatushika wengi mkatupeleke mahakamani na muende mkatufunge kwa sababu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

tutasimama na wananchi wetu npaka pale wananchi wetu mpaka pale wananchi watakuwa huru. Ni huzuni kubwa sana hata wengine wetu hapa Shella wamepewa barua wahame eti kuna bwenyenye anamiliki hapo, anamiliki kinamna gani na watu wameishi pale.

Kumekuwa na Chifu na DCC (*Deputy County Commissioner*) na watu wamejenga hawa wakiona, hivi sasa ametokea mtu anasema hii ni sehemu yake anahitaji kulipwa, analipwa kwa mambo gani? Mheshimiwa Spika mimi naunga mkono kwa dhati kufunga Bunge hili mpaka pale mheshimiwa Tete atatoka na sio kutoka tu, tutaende huko rumande ambako yuko ikiwezekana baada ya kufunga kikao cha Bunge hii. Tutakuwa huko mpaka tuhakikishe mheshimiwa Tete ametoka kwa sababu hana hatia, ni udhalilishaji ambao ulifanywa baina ya Hakimu na mabwenyenye ili waweze kumnyima dhamana mheshimiwa Tete. Naunga mkono kufungwa kwa Bunge hili. Asanteni sana.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante mheshimiwa Morris (Hinzano). Saa hii wacha tusikie kutoka kwa mheshimiwa Rashid Odhiambo akichangia mada hii.

Hon. Rashid: Thank you, Mr. Speaker. I rise to support the suspension of this honourable House indefinitely.

Mr. Speaker, Article 49(1) of the Constitution of Kenya, gives an arrested person a right to be released on bond or bail on a reasonable condition. It is our prayer that our colleague, hon. Tete is to be released on bail so that he can continue with his duty. It is so sad that we have resumed and one of us is not in. We stand in solidarity with our brother hon. Tete, and I urge the Members that all of us demonstrate and show our solidarity with hon. Tete. Hon. Members, simply if we do not do this, today is hon. Tete, tomorrow we will have so many Tetes in this House. Thank you, Mr. Speaker.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Hon. Members, there being no other business, this House stands adjourned until further communication is made.

The House rose at 3:14 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*